Uhuru, Tarehe 19/11/2020 Uk.
19

# Dk. Tamatamah aridhishwa ujenzi ofisi za uvuvi

**NA MWANDISHI WETU**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, ameeleza kuridhishwa na ujenzi wa majengo maalumu kwa ajili ya ofisi za Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU), kupitia Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH).

Amewataka makandarasi kuhakikisha majengo hayo yanakamilika ifikapo Desemba, mwaka huu, kama makubaliano yalivyo kwenye mikataba.

Dk. Tamatamah, aliyasema hayo juzi, alipofanya ziara ya kikazi ya siku mbili katika mkoa ya Pwani na Tanga, ambapo alikutana na viongozi wa BMU na wananchi kwa nyakati tofauti, baada ya kutembelea majengo hayo kwenye Kata ya Dunda, Wilaya ya Bagamoyo na Kata ya Saadani, Wilaya ya Chalinze, Mkoa wa Pwani, Kata ya Kipumbwi Wilaya ya Pangani na Kata ya Zingibari, Wilaya ya Mkinga, Mkoani Tanga.

Dk. Tamatamah, alisema ujenzi wa majengo hayo unaendelea vizuri huku akiwataka wakandarasi kuhakikisha yo yanakamilika ifikapo Desemba, mwaka huu, kama makubaliano yalivyo kwenye mikataba.

"Nimeridhishwa na ujenzi wa baadhi ya majengo hayo kupitia mradi wa SWIOFISH, lakini ninawaagiza wakandarasi kuhakikisha majengo haya yanakamilika kwa wakati ili kuanzia Januari, mwakani, yaanze kutumiwa na viongozi wa BMU, kama ofisi katika shughuli mbalimbali za kulinda rasilimali za uvuvi kwenye ukanda wa Pwani. Mkandarasi yeyote ambaye hatakamilisha jengo kwa wakati, tutamchukulia hatua," alisema.

Alibainisha kuwa mradi huo, ambao unahusisha majengo matano ya BMU, likiwemo la Kata ya Sudi, Wilaya ya Mtama, Mkoani Lindi, utakaogharimu zaidi ya sh. milioni 700, ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, hivyo kukamilika kwake kutasaidia kusimamia zaidi rasilimali za uvuvi na kutunza nyaraka muhimu.

"BMU zina matatizo ya ofisi na mmekuwa mkishiriki kutokomeza uvuvi haramu, mkikamata nyavu haramu mnaziweka wapi? Ndiyo maana tunawajengea ofisi kupitia mradi wa SWIOFISH. Nia ni ulinzi shirikishi kwa kuwapatia zana, elimu na miundombinu mbalimbali," alisema

Aidha, alisema baada wakandarasi kukabidhiwa ramani za majengo hayo Julai, mwaka huu na kutakiwa kuanza mara moja ujenzi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inayosimamia mradi wa SWIOFISH, kwa upande wa Tanzania Bara, inatarajia baada ya kukabidhiwa majengo hayo Desemba, mwaka huu, mradi utanunua pia samani na vitendea kazi vingine vya ofisi, zikiwemo kompyuta.

Alisema lengo la mradi huo unaotekelezwa katika nchi tatu za Tanzania, Msumbiji na Comoro kwa ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi ni kuwajengea uwezo wananchi, hususan jamii ya wavuvi, kusimamia rasilimali za uvuvi kupitia vikundi, ambapo kwa Zanzibar, unasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, ikiwemo taasisi ya muungano ya Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (DFSA).

Katika ziara hiyo ya kikazi ya siku mbili, Dk. Tamatamah, alisema mradi huo wa miaka sita ulioanza Juni, mwaka 2015 na kutarajiwa kukamilika Mei, mwakani, umekuwa ukiendeleza jitihada za serikali.

Alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada hizo tangu zamani kwenye maeneo yenye shughuli za uvuvi kote nchini, katika kusimamia rasilimali za uvuvi ili kutoa ajira na kuhakikisha mazao ya uvuvi yananufaisha taifa na mwananchi mmoja mmoja.

Scanned with CamScanner

UJIRANI

# Wavuvi waziangukia Kenya, Tanzania uwekaji mipaka

Burhani Yakub, Mwananchi
byakub@mwananchi.co.tz

**Mkinga.** Wavuvi wilayani hapa wameziomba Serikali za Tanzania na Kenya kushughulikia haraka mchakato wa uwekaji mipaka katika bahari ya Hindi ili waweze kuendesha shughuli zao bila kubughudhiwa.

Wametoa ombi hilo kufuatia makundi ya wavuvi wa Wilaya ya Mkinga kukamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya Sheria vya Kenya wakishtakiwa kuingia na kuvua nchi isiyo yao bila kuwa na vibali, wakati wao wanaamini wanavua kwenye eneo la Tanzania.

Katibu wa kamati ya usimamizi na udhibiti wa maliasili ya bahari wa Kijiji cha Zingibar (BMU), Athuman Hussein alitoa ombi hilo jana kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia uvuvi, Dk Rashid Tamatamah alipokuwa akizungumza na wakulima wa mwani wa kijiji hicho.

Alisema wavuvi wa Wilayani hapa na Mkoa wa Tanga wamekuwa wakikamatwa na askari wa Kenya kila wanapovua samaki katika eneo lao kwa kisingizo kwamba wamevuka mpaka wakati wao wanatambua kwamba ni Tanzania.

"Aliwahi kuja Naibu Waziri wa Wizara hii, Abdallah Ulega tena siku chache baada ya kukamatwa kundi kubwa la wavuvi Kenya, tukamshtakia akasema changamoto hiyo itakwisha kwa sababu mchakato wa kuainisha mipaka baina ya Tanzania na Kenya utafanyika lakini tunahisi kama hilo limesimama," alilalamika Athumani.

Alisema kisheria ni kwamba wakati ambao mchakato wa kuainisha mipaka unaendelea ilitakiwa wavuvi wa pande zote yaani Kenya na Tanzania wasiendelee na uvuvi hadi ufumbuzi upatikane lakini wanashangaa kuona wenzao wa nchi jirani wanaendelea.

Akizungumza baada ya kupokea malalamiko hayo, Tamatamah ambaye alikagua ujenzi wa ofisi ya BMU ya Kijiji cha Zingibar alisema amechukua changamoto hiyo na atafuatilia kujua hatua iliyofikiwa.

"Ifahamike kwa mgogoro huu unahusisha wizara mbalimbali za Tanzania na Kenya kwa hivyo niwaahidi kwamba nimechukua na naenda kuifanyia kazi ili wavuvi wetu wapate fursa ya kuvua bila kusumbuliwa," alisema Tamatamah.

Kuhusu ujenzi wa ofisi ya BMU, Kijiji cha Zingibar, Katibu huyo Mkuu aliagiza kampuni iliyopewa zabauni kuijenga kuhakikisha unakamilika Desemba 4, mwaka huu ili kamati ya BMU ipate mahala pa kufanya kazi kwa ufanisi.

Katibu huyo pia alikagua ujenzi wa ofisi ya BMU Kijiji cha Kipumbwi, nyumba za watumishi wa hifadhi ya Silikanti, Kigombe na soko la samaki la Pangani Mashariki, zote zilizojengwa kwa ufadhili wa mradi wa Swiofish.

### UJIRANI MWEMA

Suala la ujirani mwema kati ya Tanzania na Kenya kwa muda mrefu limekuwa katika majadiliano, si kwa Mkinga pekee bali katika mipaka mingine kama Horohoro, Namanga na Taveta; pamoja na Ziwa Victoria.

Kilio cha wavuvi wa wilaya ya Mkinga hakina tofauti na kile cha wavuvi wa Ziwa Victoria na bila shaka suluhisho lake linaweza kuwa sawa.

Lakini katika mipaka mingine zimekuwapo tofauti za kibiashara na sheria za kodi ambazo

zimekuwa zikilibuka mara kwa mara na kutatuliwa kwa njia mazungumzo. Katika kipindi cha corona, ulilibuka mgogoro kuhusu madereva kwenda kila upande uliotulizwa na mazungumzo.

Scanned with CamScanner